

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
مشروع تَعَلُّم الإسلام – أحكام الطهارة - سواحيلي

Samo la 3

الدرس الثالث

KUKIDHI HAJA

Miongoni mwa adabu za kukidhi haja ni kama ifuatavyo;

1. Kutanguliza mguu wa kushoto na atasema kabla ya kuingia chooni: {Bimsillah ewe mwenyezi mungu najikinga kwako kutokana na mashetani waovu wa kiume na mashetani waovu wa kike} na atasema baada kutoka: (Nakuomba msamaha wako) akitanguliza mguu wake wa kulia.

يقول قبل دخول الخلاء: (بسم الله، اللهم إني أعوذ بك من الخُبثِ والخبائثِ) ،
ويقول بعد الخروج: (غفرانك) مقدماً رجله اليمنى .

Asiwe amebeba kitu ambacho ndani yake kuna utajo wa Allah, isipokuwa ataachelea kupotea.

2. Asielekee kibla wala kukipa mgongo kibla wakati wa kukidhi haja kwenye sehemu ya wazi, ama sehemu ya nyumba inafaa kukipa mgongo kibla bila ya kukielekea.

3. Kujisitiri tupu kutoka kwenye macho ya watu na kutobweteka kwenye hilo, na tupu ya mwanamume ni kuanzia kitovuni mpaka magotini na tupu ya mwanamke ni mwili wake wote.

4. Kujihifadhi na kujiepusha mwili wake au nguo zake kupatwa na mkojo au kinyesi.

5. Kujisafisha na maji baada ya kukidhi haja au kutumia tishu au mawe na mfano wake kwa ajili ya kuondoa athari ya najisi kwa kutumia mkono wake wa kushoto katika kujisafisha.